

Kanuni ya **kufunga na kuomba** inafananishwa na kanuni ya **Kuku** kuyaatamia mayai yake mpaka kufikia hatua ya kutotoa vifaranga.

Ili mayai yaweze kuanguliwa na vifaranga kutokea ni lazima Kuku ayaatamie mayai kwa **siku 21**, na ili aweze kuyaatamia kwa mafanikio, basi hana budi kujizuia kula kwa kipindi kirefu ili asipoteze joto la mayai yale. Ndio hapo utaona itampasa atoke mara chache chache kwenda kutafuta chakula kisha kuyarudia mayai yake, na atafanya hivyo kwa siku **zote 21**.

Maana yake kama kuku hatajiingiza katika hiyo adhabu ya kuutesa mwili wake na kujizuia na milo kwa siku 21, hawezi kupata vifaranga!.

Vile vile kuna mambo ambayo yanahitaji **“Joto la kiroho”** kwa siku kadhaa za **MIFUNGO na MAOMBI na KUJITESA**. Ili tuweze kuyapata...Vinginevyo hayatatokea kabisa haijalishi tutayatamani kiasi gani!.

**Bwana YESU alisema mambo mengine hayatoki pasipo Maombi na Mifungo..**

*Mathayo 17:21 “[Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga.]”*

- > Ukiona umejaribu kutafuta kitu na hujakipata, ingia kwenye mfungo!
- > Ikiwa umeomba na bado hujapata, ongezea na mfungo juu yake!.
- > Ikiwa umetafuta na hujapata ongezea na mfungo wa maombi juu yake!.
- > Ikiwa unataka Amani, Furaha, au Nguvu za kuendelea mbele, usikwepe mfungo! N.k

Ukiwa ni mtu wa kuomba pamoja na kufunga, utakuwa ni mtu wa mafanikio kiroho na kimwili. Utaangua vingi kwa wakati.. Lakini ukiwa ni mtu wa kukwepa mifungo basi utatumia nguvu nyingi sana kupata baadhi ya mambo.

*Danieli 9:2 “katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, mimi Danielii, kwa kuvisoma vitabu, nalifahamu hesabu ya miaka, ambayo neno la Bwana lilimjia Yeremia nabii, ya kuutimiza ukiwa wa Yerusalemu, yaani, miaka sabini.*

*3 Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka KWA MAOMBI, na dua, PAMOJA NA KUFUNGA, na kuvaa nguo za magunia na majivu.....*

*21 naam, nilipokuwa nikinena katika kuomba, mtu yule, Gabrieli, niliyemwona katika njozi hapo kwanza, akirushwa upesi, alinigusa panapo wakati wa dhabihu ya jioni.*

*22 Akaniagiza, akaongea nami, akasema, Ee Danielii, nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu.*

*23 Mwanzo wa maombi yako ilitolewa amri, nami nimekuja kukupasha habari; maana wewe unapendwa sana; basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya”.*

Na kuna Toba nyingine zinahitaji Mfungo kabisa ili mtu aweze kufunguliwa.

*Yoeli 2:12 “Lakini hata sasa, asema Bwana, nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea;*

*13 rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, mkamrudie Bwana, Mungu wenu; kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, naye hughairi mabaya”.*

Usikwepe mifungo!

Shalom.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

**Mafundisho mengine:**

Kwanini tunafunga na kuomba?

**Je unaruhusiwa kufanya tendo la ndoa ukiwa katika mfungo?**

**HIZI NI NYAKATI ZA KUFUNGA NA KUOMBA.**

**Kuomba katika roho ni kupi? na je nifanye nini ili niweze kuomba hivyo?**

**NJIA SAHIHI YA KUFUNGA.**

**IJUE FAIDA YA KUFUNGA PAMOJA NA WANYAMA WAKO.**

**Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp

[Print this post](#)